
# Mshangilieni Mungu enyi Inchi zote

Zaburi 65

Mus : Innoncent BISHIKWABO




1. Mshangilieni Mungu, enyi inchi zote,
   uimbeni utukufu wa jina lake, mtoleeni sifa tukufu.
   Mwambieni Mungu : "Matendo yako
   jinsi yalivyo yakutisha.

2. Dunia nzima ikuabudu na kukuimbia,
   iliimbie jina lako.
   Njoni, tazameni matendo ya Mungu:
   amefanya ya kutisha kati ya wanadamu.

3. Aligeuza bahari kuwa nchi kavu;
   watu walivuka mto kwa miguu:
   kwa hiyo twataka kumfurahia.
   Atawala kwa ezi yake hata milele.

4. Njoni, sikieni, wote mnaomheshimu Mungu,
   nitawaelezea makuu aliyonitendea roho yangu.
   Asifiwe Mungu: hakunyima maombi yangu,
   wala hakuepusha nami wema wake.